

5 HABARI

MALENG&gt;&gt;

# NARCO yatangaza mipango ya kuinua wafugaji nchini

Na JACQUELINE MASSANO

**M**ENEJA Mkuu wa Kampuni za Ranchi za Taifa (NARCO), Profesa Peter Msosse, ametaja mikakati itakayosalida kampuni hiyo, kuweza kujijendesha kibashara zaidi na kusaidia wafugaji nchini kufuga kisasa.

Mikakati hiyo, alitaja mwishoni mwa wiki baada ya kumalizika kwa kikao cha makabidhiano ya ofisi na aliyekuwa Kaimu Meneja Mkuu wa NARCO, Masele Shilagi, kilichofanya katika ofisi za kampuni hiyo zilizopo jijini Dodoma.

Alitaja mikakati hiyo kuwa serikali inataki kampuni hiyo, iwe kitovu cha umahiri wa masuala yote yanayohusu ranchi.

Msosse alisema katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, ni lazima kampuni ijjipange kuzalisha nyama ya kutosha na ilio bora, uzalishaji wa mifugo iliyobora, kutoa

mafuzo kwa wataalamu na wafugaji, kujijendesha kibashara na kuweza kupeleka gawio senkalini.

Alisema ana matarajio makubwa, kuwa hayo yatawezekana kwa kuwa ameikuta kampuni ikiwa inaendelea kuimariaka hivyo kwa kushirikiana na viongozi na watendaji wa kampuni wataweza kutekeleza mikakati hiyo, ambayo itawasaidia kutimiza azma ya serikali kwa kampuni hiyo.

Naye, aliyekuwa Kaimu Meneja wa NARCO, Shilagi, alisema kampuni imekuwa ikiendelea kuimariaka kimapato na kuwa iliweza kujijendesha bila kutumia ruzuku kutoka serikalini.

"Pia tumeweza kusimamia mapato na matumizi, kampuni imekuwa ikipata hati safi," alisema.

Pia, alisema kampuni imeweza kupirma baadhi ya ranchi zake na kushughulikia migogoro iliyokuwepo, ikiwemo ya uvamizi

wa wananchi katika maeneo ya ranchi.

Aidha, Masele aliwashukuru viongozi na watumishi wa NARCO kwa ushirikiano waliompatia kipindi cha uongozi wake na kwaomba waendelee kutoa ushirikiano kwa Meneja Mkuu mpya.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Uzalishaji na Masoko, Stephen Michael, alisema viongozi na watendaji, wanao wajibu wa kujipanga vizuri ili kuhakikisha malengo na matarajio ya serikali yanatimizwa.

"NARCO inazo fursa nyingi katika uzalishaji wa nyama bora, mifugo bora, malisho na utoaji wa elimu kwa wafugaji," alisema.

Alisema katika kuhakikisha fursa zinatumika na mapato yanaongezeka kama serikali iliyopanga, ni lazima uongozi uone namna bora ya kushirikiana na sekta binafsi lengo likiwa ni kuongeza uzalishaji na mapato.

Waajiri  
kuweka  
salama se

Na REHEMA M

WAKALA wa U  
Mahall Pa Kaz  
waajiri nchini i  
sehemu ya kaz  
zaidi.

Akizungum  
katika viwanja  
ya Kimataifa  
vya Mwalimu  
Ofisa Habab  
Gyuna, alisen  
ni muhimu i  
Inaleta tija ya

Gyuna al  
wao, sehemu  
wanaona  
sehemu za  
iliyyokuwa t

Alisema  
changamoto  
elimu inay  
maofisa w  
sehemu za  
"Kuna  
kufuata s  
kazi, ili ut  
kwa ajili

## MAKABIDHIANO

MENEJA Mkuu  
wa Kampuni  
ya Ranchi za  
Taifa (NARCO),  
Profesa Peter  
Msosse (kulia),  
akipokea  
nyaraka  
za ofisi  
kutoka kwa  
aliyekuwa  
Kaimu Meneja  
Mkuu wa  
kampuni hiyo,  
Masele Shilagi,  
jijini Dodoma.  
Katikati  
ni Kaimu  
Mkurugenzi  
wa Uzalishaji  
na Masoko  
katika Wizara  
ya Mifugo  
na Uvuvi,  
Stephen  
Michael.

